

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



MKUU WA TAKUKURU MKOA  
Mtaa wa Uzunguni,  
S.L.P 37,  
37101 SHINYANGA,  
Tanzania.  
Simu: (028) 2762630  
Nukushi: (028) 2763358

---

FEBRUARI 10, 2021.

**TAKUKURU MKOA WA SHINYANGA**  
**MWALIMU ATIWA HATIANI KWA KOSA LA KUHUFUJUMU UCHUMI.**

Leo tarehe 10/02/2021 ofisi ya TAKUKURU mkoani Shinyanga kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, imemfikisha katika mahakama ya wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mwalimu Wilfred Emanuel Manumbu kwa makosa ya mawili, kosa la kwanza ni wizi akiwa mtumishi wa umma ambapo anatumwiwa kumwibia mwajiri wake ambaye ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiasi cha sh 10,947,400/= na kosa la pili ni kumsababishia hasara mwajiri wake ambaye ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiasi cha sh. 10,947,400/=.

Katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 07/2021 mshtakiwa alikiri kutenda makosa hayo ambayo aliyafanya kati ya mwezi Oktoba 2013 na Januari 2016 huko katika Halmashauri ya wilaya ya Ushetu alikokuwa ameajiriwa kama Mwalimu wa Shule ya Msingi Nyaweshi.

Mshtakiwa alikiri makosa yake na mahakama imemtia hatiani kwa makosa yote mawili na kumhukumu kwenda jela miaka mitatu (03) na kulipa fedha zote alizohujumu kiasi cha sh. 10,947,400/=

Natoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Shinyanga kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU ili kuhakikisha kuwa tunaondoa kero za rushwa katika mkoa wetu wa Shinyanga.

**Imetolewa na H.M MUSSA, Mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Shinyanga.**